Maovu Mawili Makuu

na

Ellis P. Forsman

Maovu Makuu Mawili

Na

Ellis P. Forsman

October 15, 2011

Maovu Makuu Mawili

Yeremia 2:13

Miaka 600 kabla ya Kristo, taifa la Yuda lilikuwa linakumbana na wakati mgumu…

Ufalme wa kaskazini ya Israeli ilikuwa historia, ikapelekwa katika utumwa Ashuru.

Manase na mwanaye Amnoni, mfalme mwovu, aliongoza taifa katika kuabudu sanamu.

Kijana Yosia, mwana na mjukuu wa wafalme wa aina hiyo, alijitahidi kufanya kilichokuwa sahihi.

Katika mwaka wa kumi na tatu wa utawala wa Yosia, Mungu alimwita kijana kuhani ili awe nabii wake.

Jina lake aliitwa Yeremia.

- Yer. 1:1-2, "*Maneno ya Yeremia mwana wa Hilkia, mmoja wa makuhani waliokuwa katika Anathothi, katika nchi ya Benyamini; ambaye neno la BWANA lilimjia katika siku za Yosia, mwana wa Amoni, mfalme wa Yuda, katika mwaka wa kumi na tatu wa kumiliki kwake.*"

- Yer. 1:4-5, "*Neno la BWANA lilinijia kusemaa, kabla sijakuumba katika tumbo nalikujua, na kabla hujatoka tumboni nalikutakasa; nimekuweka kuwa nabii wa mataifa.*"

Kijana mdogo mwenyewe (kama miaka 20), alikuwa na uwezo wa kunena.

Yer. 1:6, "*Ndipo niliposema, Aa, Bwana MUNGU! Tazama siwezi kusema maana mimi ni mtoto.*"

Mungu hakuukubali utoto wake kama kigezo.

Yer. 1:7-8, "*Lakini BWANA akaniambia usiseme, mimi ni mtoto; maana utakwenda kwa kila mtu nitakayekutuma kwake, nawe utasema kila neno nitakalokuamuru. Usiogope kwa sababu ya hao maana mimi nipo pamoja nawe nikuokoe, asema BWANA.*"

Katika majukumu yake ya kwanza kama nabii wa Mungu, Yeremia alitumwa na ujumbe katika…

Yerusalemu, akikumbuka uaminifu wao wa zamani.

Yer. 2:1-3, "*Neno la BWANA likanijia kusema, enenda ukalie masikioni mwa Yerusalemu, ukisema BWANA asema hivi, nakukumbuka hisani ya ujana wako, upendo waa wakati wa uposo wako; jinsi ulivyonifuata huko*

jangwani, katika nchi isiyopandwa mbegu. Israeli walikuwa utakatifu kwa BWANA; malimbuko ya uzao wake; wote watakaomla watakuwa na hatia; uovu utawajilia asema BWANA."

Nyumba ya Yakobo na jamii zote za nyumba ya Israeli, waliomboleza kuhusiana na upotovu wao katika kuabudu sanamu.

Yer. 2:4-11, "*Lisikieni neno la BWANA, ninyi nyumba ya Yakobo, na ninyi jamaa zote za nyumba ya Israeli. BWANA asema hivi, bab zenu waliona dhuluma gani kwangu, hata wakafarakana nami, wakafuata ubatili, nao wakawa ubatili? Wala hawakusemaa yuko wapi BWANA, aliyetutoa katika nchi ya Misri; akatuongoza jangwani, katika nchi ya ukame na mashimo, katika nchi ya kiu na ya kivuli cha mauti, katika nchi ambayo ndani yake hapiti mtu, wala haikukaliwa na watu? Nami nikawatia katika nchi ya shibe, mpate kula maatunda yake na mema yake; lakini ninyi mlipoingia katika nchi ile, mliitia unajisi nchi yangu, na urithi wangu mliufanya kuwa chukizo. Makuhani hawakusema yuko wapi BWANA? Wala wanasheria hawakunijua; wachungaji nao waliniasi, nao manabii walitoa unabii kwa Baali, wakafuata mambo yasiyofaidia kitu. Basi kwa ajili ya hayo nitateta nanyi, asema BWANA, nami nitateta na watoto wa watoto wenu. Maana vukeni mpaka visiwa vya Kitimu, mkaone; tumeni watu waende Kedari, mkafikiri sana; mkaone kwamba jambo kama hili limekuwa wakati wowote. Je! Taifa limebadili miungu yao, ingawa siyo miungu? Lakini watu wangu wameubadili utukufu wao kwa ajili ya kitu kisichofaidia.*"

Wito wa mbingu kustaajabu na uoga mkuu, Mungu alipowashutumu watu wake walipotenda maovu makuu mawili.

Yer. 2:12-13, "*Enyi mbingu, staajabuni kwa ajili ya jambo hili, mkaogope sana na kuwa ukiwa sana, asema BWANA. kwa maana watu wangu hawa wametenda maovu mawili; wameniachaa mimi niliye chemchemi ya maji ya uzima, wamejichimbia mabirika, mabirika yavujayo, yasiyowezaa kuweka maji.*"

Wakimwacha Mungu wao, chemchemi ya maji yao ya uzima.

"*Maji yaliyo hai*" ilitumiwa kuonyesha chemchemi, bubujiko la maji, maji yanayo tiririka mferejini.

Ikitofautishwa na maji yaliyotulia na kusimama.

Wakijichimbia mabirika yanayovuja ambayo hayawezi kubeba maji.

Mabirika yalitumika kuhifadhi maji ya mvua, hasa (hukatwa) kutoka kwenye jiwe.

Kwa ubora, zinaweza tu kutoa maji yaliyosimama.

Yana matundutundu, hayawezi hata kushikiliaa maji.

Je tunaweza kuwa na hatia ya uovu unaofanana na huo leo? Kwa hofu ya Mungu na uovu wetu wenyewe, zaidi sana! Kuona ni jinsi gani, ebu tuangalie kwa kaaribu "*Maovu makuu mawili*" yaliyonenwa katika Yer. 2:13.

Kuacha chemchemi ya maji ya uzima

Israeli iliacha chemchemi yake.

Mungu alikuwa chemchemi ya maji ya uzima ya Israeli.

Yer. 2:6-7, "*Wala hawakusemaa yuko wapi BWANA, aliyetutoa katika nchi ya Misri; akatuongoza jangwani, katika nchi ya ukame na mashimo, katika nchi ya kiu na ya kivuli cha mauti, katika nchi ambayo ndani yake hapiti mtu, wala haikukaliwa na watu? Nami nikawatia katika nchi ya shibe, mpate kula maatunda yake na mema yake; lakini ninyi mlipoingia katika nchi ile, mliitia unajisi nchi yangu, na urithi wangu mliufanya kuwa chukizo.*"

Aliyewatoa utumwani Misri.

Aliyewaongoza jangwani.

Aliyewatia katika nchi ya maziwa na asali.

Israeli ilimsahau Mungu wake.

Ukianza na manabii wake mwenyewe na watawala.

Yer.2:8, "*Makuhani hawakusema yuko wapi BWANA? Wala wanasheria hawakunijua; wachungaji nao waliniasi, nao manabii walitoa unabii kwa Baali, wakafuata mambo yasiyofaidia kitu.*"

Kutoka kizazi kimoja haadi kingine.

Yer. 2:9, "*Basi kwa ajili ya hayo nitateta nanyi asema BWANA, nami nitateta na watoto wa watoto wenu.*"

Kama mataifa mengine yalivyokuwa kweli kwa miungu yao.

Yer.2:10-11, "*Maana vukeni mpaka visiwa vya Kitimu, mkaone; tumeni watu waende Kedari, mkafikiri sana; mkaone kwamba jambo kama hili limekuwa wakati wo wote. Je! Taifa wamebadili miungu yao, ingawa sio miungu? Laakini watu wangu wameubadili utukufu wao kwa ajili ya kitu kisichofaidia.*"

Israeli walibadili Utukufu wao (Mungu) kwa kile ambacho kilikuwa hakifaidii!

Tunaweza kuthubutu kuiacha chemchemi yetu?

Tuna chemchemi yetu ya maji ya uzima.

Ambayo Yesu alihaidi wakati wa utumishi wake…

Kwa mama Msamaria.

Yohan 4:13-14, "*Yesu akajibu, akamwambia, kila anyway maji haya ataona kiu tena; walakini yeyote atakeyekunywa maji yale nitakayompa mimi hataona kiu milele; bali yale maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele.*"

Kwa wote wanaomwamini.

Yohana 7:37-39, "*Hata siku ya mwisho, siku ile kubwa ya sikukuu, Yesu akasimama akapaza sauti yake akisema, mtu akiona kiu aje kwangu anywe. Aniaminiye mimi, kama vile maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake. Na neno hilo alilisema katika habari ya Roho, ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye; kwa maana Roho alikuwa hajaja, kwa sababu Yesu alikuwa hajatukuzwa.*"

Ambayo baadae Yesu alimfunulia mtume Yohana…

Kuzingatia hali yetu kati ya kifo na mauti.

Ufu. 7:13-17, "*Akajibu mmoja wa wale wazee akiniambia, Je! Watu hawa waliovikwa mavazi meupe ni akina nani? Na wametoka wapi?Nikamwambia, Bwana wangu wajua wewe. Akaniambia hao ndio wanatoka katika dhiki ile iliyo kuu, nao wamefua mavazi yao na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo. Kwa hiyo wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, nao wanamtumikia mchana na usiku katika hekalu lake, na yeye aketiye katika kiti cha enzi atatanda hema yake juu yao. Hawataona njaa tena, wala hawataona kiu tena, wala jua halitawapiga, wala hari iliyo yote. Kwa maana huyo Mwana-Kondoo, aliye katikati ya kiti cha enzi, atawachunga, naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uhai, na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao.*"

Kuzingatia hatima yetu ya milele katika Yerusalemu mpya.

Ufu. 22:1, "*Kisha akanionyesha mto wa maji ya uzima, wenye kung'aa kama bilauri, ukitoka katika kiti cha enzi cha Mungu, na cha Mwana-Kondoo.*"

Tunathubutu kumuacha Mungu wetu?

Ambaye kupitia Yesu na Roho wake ametupatia katika maisha haya:

Chemchemi ya maisha ya milele?

Yohana 4:14, "*Walakini ye yote atakaye kunywa maji yale nitakayompa mimi hataona kiu milele; bali yale maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele.*"

Mito ya maji yaliyo hai yakitirirka kutoka katika mioyo yetu?

Yohana 7:38, "*Aniaminiye mimi kama vile maandiko yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake.*"

Ambaye kupitia Yesu na Roho wake ametuahidia baada ya maisha haya:

Kutuongoza katika chemchemi ya maji?

Ufu. 7:17, "*Kwa maana huyo Mwana-Kondoo, aliye katikati ya kiti cha enzi, atawachunga, naye atawaongoza kwenye chemchemi za maji yenye uhai, na Mungu atayafuta machozi yote katika macho yao.*"

Mto ulio na maji masafi ya uzima, ukitoka katika kiti cha enzi ya Mungu?

Ufu. 22:1, "*Kisha akanionyesha mto wa maji ya uzima, wenye kung'aa kama bilauri, ukitoka katika kiti cha enzi cha Mungu, na cha Mwana-Kondoo.*"

Tunakabiliana na uwezekano halisi wa kumuacha Mungu aliye hai!

Heb. 3:12-14, "*Angalieni ndugu zangu, usiwe katika mmoja wenu moyo mbovu wa kutokuamini, kwa kujitenga na Mungu aliye hai. Lakini mwonyane kila siku, maadamu iitwapo leo; ili mmoja wenu asifanywe mgumu kwa udanganyifu wa dhambi. Kwa maana tumekuwa washirika wa Kristo, kama tukishikamana na mwanzo wa uthabiti wetu kwa nguvu mpaka mwisho.*"

Kuacha chemchemi yetu ya maji yaliyo hai inatokea tunapoibadili kwa yenyewe "mabirika yanayovuja ambayo yanahaidi lakini hayatowi. Kumbuka ambacho Yuda alifaanya…

Mabirika yavujayo yasiyoweza kubeba maji

Israeli walikuwa na birika lililotoboka…

miungu ya uongo kama Baali.

Yer. 2:8, "Makuhani hawakusema yuko wapi BWANA? Wala wanasheria hawakunijua; wachungaji nao waliniasi, nao manabii walitoa unabii kwa Baali, wakafuata mambo yasiyofaidia kitu."

Manabii wa uongo walionena kwa jina la Baali.

Fikra potofu ya mafanikio, ambayo Mungu alionya kabla.

- Kumb. 8:11-17, "*Jihadhari, usije ukamsahau BWANA, Mungu wako, kwa kutozishika amri zake, na huku zake, na sheria zake, ninazokuamuru leo. Angalia utakapokuwa umekula na kushiba, na*

kujenga nyumba nzuri na kukaa ndani yake; na makundi yako ya ng'ombe na kondoo yatakapoongezeka, na fedha yako na dhahabu yako itakapoongezeka, na kila kitu ulichonacho kitakapoongezeka; basi hapo moyo wako usiinuke, ukamsahau BWANA Mungu wako, aliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa; aliyekuongoza katika jangwa lile kubwa lenye kitisho, lenye nyoka za moto na nge, nchi ya kiu isiyokuwa na maji; aliyekutoleaa maji katika mwamba mgumu, aliyekulisha jangwwani kwa mana, wasioijua baba zako; apate kukutweza, apate kukujaribu, ili kukutendea mema mwisho wako. Hapo usiseme moyoni mwako, Nguvu zangu na uwezo wa mkono wangu ndio ulionipatia utajiri huo."

- Yer. 2:6, "*Wala hawakusema yuko wapi BWANA, aliyetutoa katika nchi ya Misri; akatuongoza jangwani katika nchi ya ukame na mashimo, katika nchi ya kiu na yaa kivuli cha mauti, katika nchi ambayo ndani yake hapiti mtu, wala haikukaliwa na watu?*"

Israeli walimuacha Mungu kijinga kwa ambacho kilikuwa mbadala mbovu!

Je tunajichimbia mabirika yanayovuja?

Tunaweza kuwa na hatia ya kuziendea miungu leo.

- Efe. 5:5, "*Mana neno hili mnalijua hakika, ya kwamba hakuna mwasherati wala mchafu wala mwenye tamaa, ndiye mwabudu sanamu, aliye na urithi katika ufalme wa kristo na Mungu.*"

- Kol. 3:5, "*Basi vifisheni viungo vyenu vilivyo katika nchi, uasherati, uchafu, tamaa mbaya, mawazo mabaya, na kutamani, ndiyo ibada ya sanamu;*"

Mambo ya kimwili naa uchafu ulioje.

Ambayo ipo kwa jinsi ya sanamu.

Tunaweza kuwa na hatia ya kuwasikiliza manabii wa uongo (waalimu).

2 Pet. 2:1-3, "*Lakini kuliondokea manabii wa uongo katika wale watu, kama vile kwenu kutakavyokuwako waalimu wa uongo, watakaoingiza kwa werevu uzushi wa kupoteza, wakimkana hata Bwana aliyewanunua, wakijileteaa uharibifu usiokawia. Na wengi watafuata ufisaidi wao; na kwa hao njia ya kweli itatukanwa. Na katika kutamani watajipatia faida kwenu kwa maneno yaliyotungwa; ambayo hukumu yao tangu zamani haikawii, wala uvunjifu wao hausinzii.*"

Nani anayetuongoza katika udhehebu au mgawanyiko.

Kinyume na sala ya Yesu na umoja wa Roho.

- Yohana 17:20-21, "*Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao. Wote wawe na umoja kama wewe Baba, ulivyo ndani yangu nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma.*"

- Efe. 4: 3-6, "*Na kujitahidi kuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani. Mwili mmoja, Roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu. Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja. Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote.*"

Wengine wanaowapa watu matumaini ya uongo: mazingaombwe, dini za uongo, wanaodanganya watu kuwa matari haraka.

Tunaweza kuwa na hatia kwa dhana potofu ya mafanikio.

Ufu. 3:17-18, "*Kwa kuwa wasema mimi ni tajiri, nimejitajirisha wala sina haja ya kitu; nawe hujui ya kuwa wewe u mnyonge, na mwenye mashaka, na maskini, na kipofu, na uchi. Nakushauri ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto upate kuwa tajiri, na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako isionekane, na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona.*"

Tukiamini tuko salama kiroho...

Tunapokuwa katika hatari ya kaburi ya kushindwa.

1 Kor. 10:12, "*Kwa hiyo anayejidhania kuwa amesimama na aangalie asianguke.*"

Tunaweza kuwa na hatia ya kumuacha Mungu kwa mbadala mbovu wa dini ya kweli!

Hitimisho

Maovu mawili yaliyotendwa na Israeli…

Kwanza, walimuacha Mungu, Chemchemi ya uzima, mwanga, na furaha.

Pili, walijichimbia mabirika mabovu; walijiingiza wenyewe katika sanamu, ambapo wangepata mema yao ya kiroho ya muda mfupi!

Matendo yao yalizidi uharibifu na upofu.

Inaweza kuwa zaidi kiasi gani kama tukiwa na matendo mabovu na upofu…

Kumuacha Mungu, Yesu, na Roho Mtakatifu, kwa kuacha kujitoa kwetu na utii wa neno la Mungu!

Kutumia muda mwingi kunywea “birika lililotoboka” (mafundisho na maagizo ya wanadamu), kuliko chemchemi ya maji yaliyo hai (Neno la Mungu lililo hai).

Mfano huu mbaya wa Yuda utumike kama onyo kwetu kwamba ni wapi tupate “maji” yetu, na tuwe wazi kwa mwaliko huu wa ajabu uliotolewa mwishoni mwa kitabu cha Ufunuo:

Ufu. 22:17, “*Na Roho na Bibi arusi wasema njoo! Naye asikiaye na aseme njoo! Naye mwenye kiu na aje; na yeye atakaye, naa ayatwae maji ya uzima bure.*”

Je “*unakunywa maji ya uzima*”, au katika birika lililotoboka ambalo haliwezi kubeba maji”?